KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 16, Issue 1

8th Dhul Hijjah 1432

4th Nov, 2011

YALIYOMO

SWALA YA 'EID NA HUKMU ZAKE 1 - 4

'EID MBILI NA HUKMU ZAKE

Na: Sheikh AbdulMajeed Alee Hasan.

ADABU YA MUISLAMU KATIKA SIKU YA 'EID-UL- ADH-HAA:

Katika kukadiria mawazo ya kujitafautisha na Washirikina, ni jambo lenye umuhimu sana kusema yakwamba: Kwa mujibu wa kuwa tafauti kwenye sherehe zetu kulingana na alivyotufundisha Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم), hatuna budi kuifuata Sunnah kama ilivyo. Jambo hilo litatupelekea sisi kufanya amali za kuwa wafuasi halisi wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwahiyo, iwapo sisi tutataka kuwa ni wafuasi wake (صلى الله عليه وسلم), ni lazima tutahadhari na Bid'ah. Bid'ah hutokeza kwa gharama za Sunnah inayochukuwa nafasi yake. Amesema Ibn Taymiyyah kwenye kitabu chake, *al-Iqtidhaa':* "Hapana nafasi kwenye Moyo ya Bid'ah na Sunnah pamoja."

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Sema: 'Ikiwa nyinyi mnampenda Allaah, basi nifuateni; (hapo) Allaah atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu."** [Aali 'Emraan: 31]

Kila Muislamu anahitajika kufuata mafunzo ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kabla hajenda katika Swala ya 'Eid. Ni muhimu sana kufuata Sunnah za 'Eid ili tuwe ni wenye kusema kwa uhakika yakwamba sherehe zetu ni tafauti na sherehe za washirikina.

SUNNAH ZA 'EID KWA KILA MWENYE KUHUDHURIA SWALA YA 'EID:

1. Muislamu anawajibika kutekeleza Ghusl (kuoga) au atawadhe katika siku hiyo. Jambo hilo (la kuoga) linaweza kufanywa wakati wowote, lakini makusudio yaliyoazimiwa imependekezwa kutekelezwa kabla ya kutoka na kuelekea kwenye musalla. Swala ya 'Eid huswaliwa kwa jamaa na hutekelezwa na mkusanyiko mkubwa wa watu zaidi ya swala ya Ijumaa. Kwahivyo, kwa vile Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahimiza Waislamu waoge kwa swala ya Ijumaa, inahitaji pia kuzingatiwa kwa swala ya 'Eid ili yapatikane malengo. Malengo na makusudio ni kuwa mswafi kwa ajili ya swala na kujiepusha kuwadhuru watu kwa harufu chafu ,n.k (na kadhaalika). Imaam al-Baghawee amesema katika kitabu chake, Sherh as-Sunnah vol.4, Uk.301-302, yakwamba, "Na Sunnah ni kuoga katika siku ya 'Eid. Imepokewa yakwamba Ali (رضي الله عنه) alikuwa akioga siku ya 'Eid, na vilevile imepokewa yakwamba Ibn 'Umar (رضي الله عنه) na Salamah Ibn al-Akwa walikuwa wakifanya hivyo." Riwaya ya Ali inapatikana katika kitabu cha Imaam ash -Shaafi'ee: Musnad Ash-Shaafi'ee: vol.1, Uk.168, lakini riwaya hii si swaheeh kutokana na Ibraaheem ibn Muhammad ambaye ni dha'eef kulingana na rai ya Wanavyuoni wa hadeeth. Riwayaq nyengine ya Ibn 'Umar inapatikana kwenye kitabu cha Imaam Maalik: al-Muwatta': (cha Kiarabu) vol: 1, Uk.177 na (Tafsiri ya Ki-Ingereza): Uk.84, mlango:104, hadeeth: 421. Itafute kwenye Zaad ul Ma'aad vol. 1, Uk. 441-2.

2. Kula katika siku Mbili za 'Eid: Ni Sunnah kula tende kabla ya kutoka na kuelekea kwenye musalla kwa ajili ya 'Eid ul-Fitr. Imependekezwa kuto kula kitu chochote kabla ya kutoka na kuelekea kwenye musalla kwa ajili ya 'Eid ul-Adh-ha mpaka baada ya kuswali swala ya 'Eid asubuhi. Kisha mtu na arudi nyumbani, achinje mnyama na atayarishe chakula na ale kutokana na kichinjo hicho. Kwa 'Eid ul-Fitr, ni Sunnah kula tende kwa idadi isiyogawanyika kwa mbili kabla ya kwenda kuswali swala ya 'Eid, haliyakuwa kwa 'Eid ul-Adh-ha, kula na kucheleweshwe mpaka mtu arudi kutoka kwenye swala ya 'Eid, kisha anaweza kula kutokana na kichinjo chake iwapo atakuwa amechinja mnyama. Amepokea Anas: "Mtume (صلى الله عليه وسلم), hakuwa ni mwenye kutoka kuelekea kwenda kuswali katika siku kuu ya kufungua saumu mpaka kwanza ale tende kwa idadi isiyogawanyika kwa mbili." Swaheeh al-Bukhari: vol. 2, no.73.] Amepokea Buraidah: "Mtume (صلى الله عليه وسلم), hakuwa ni mwenye kutoka katika siku ya kufungua saumu ('Eid ul -Fitr) mpaka kwanza awe ashakula na katika siku Kuu ya kuchinja ('Eid ul-Adh-ha), hakuwa akila mpaka arudipo kutoka kwenye musalla. Hili limepokewa na at-Tirmidhee na Ibn Maajah na pia na Sunan ad-Daarimee aliyekuwa na nyongeza isemayo: "Na alikuwa akila kutokamana na kichinjo chake." [Sharhus Sunnah: vol. 4, Uk. 306, nukta za chini: 1]

3. Imependekezwa mno yakwamba na avae katika nguo zake nzuri siku hiyo. Amepokea Ja'far Ibn Muhammad kutoka kwa babake kutoka kwa babu yake aliyepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akivaa kilemba cha ki-Yemen katika kila 'Eid. Yamepokewa hayo na Ash-Shaafi'ee na al-Baghawee. Amenukuu Ibn al-Qayyim: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akivaa katika nguo zake nzuri zaidi na alikuwa na kilemba ma'lum ambacho alikuwa akivaa kila ifikapo 'Edi mbili na Ijumaa. and he had a special cloak that he would wear on the two 'Eids and Jumu'ah. [Sharhus Sunnah: vol. 4, Uk. 302, nukta za chini. 2. Angalia Zaadul Mi 'a ad: vol. 1, Uk.441]

4. Na anahitajika atumie mafuta ya nywele.

5: Anahitajika ajitie mafuta ya manukato iwapo atakuwa nayo yake mwenyewe, au vyenginevyo, aweza kutumia mafuta ya mkewe. Al-Hassan as-Sibt amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametuamrisha sisi tijivalie nguo bora tuwezazo kujipatia

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

kwa 'Eid mbili na kujitie manukato yaliyo bora tuwezayo kujipatia na tujichinjie mnyama aliye bora tuwezae kumpata. Haya yamepokewa na al-Haakim na kwenye silsila yake kuna Is-haaq ibn Barzakh ambaye al-Azdi alimthibitisha kuwa ni dha'eef haliyakuwa ibn Hibbaan amesema yakuwa ni mwenye kuaminika.

6. Anatakiwa atumie msuaki kabla hajenda kuswali swala ya 'Eid.

7. Ni lazima ajisafishe na harufu zote mbaya zenye uwezo wa kuwaletea madhara wengine. Ni haramu kwake kuhudhuria swala ya 'Eid ikiwa atakuwa na harufu za vitunguu na Thomo.

TANABAHI: Sunnah zote hizi zilizotajwa hapo juu zinazingatiwa sawa na Sunnah za Swala ya Ijumaa kwa sababau madhumuni ya kuzihifadhi ni sawa na yale ya Ijumaa.

Swala ya 'Eid inaweza kutekelezwa kwenye msikiti lakini imependeke3zwa kuswaliwa mahali ambapo ni nje ya Mji maadamu hakuna pingamizi au sababu ya kufanya kinyume cha hivyo (kwa mfano Mvua). Kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali 'Eid mbili pambizoni mwa Mji wa al-Madeenah na wala hakuswali msikitini, isipokuwa iliwahi kupokewa kwa njia ya riwaya dha'eef yakwamba wakati mmoja aliswali msikitini kwa sababu ilikuwa kukinyesha.

TAKBEERAT KATIKA SIKU ZA 'EID

Ni Sunnah kuzisoma takbeerat katika siku za 'Eid kwa sauti ya juu. Kuhusiana na 'Eid ya Siku ya 'Eid ul-Fitr, Allaah amesema: **"Na pia (anakutakieni) mtimize hisabu hiyo, na (anakutakieni) kumtukuza Allaah [kutamka Takbeerat] kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru." [**Al-Baqarah: 2: 185**]** Amma kuhusu 'Eid ya kuchinja, Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"... Na kulitaja jina la Allaah katika siku zinazojulikana..."** [al-Hajj 22: 28]. Kundi kubwa la wanavyuoni wamesema yakwamba nyakati za Takbeeraat katika 'Eid ul-Fitr ni kuanzia wakati mtu anapokwenda kwenye swala ya 'Eid mpaka ianzapo khutbah.

Ahaadeeth dha'eef zenye kusema haya zimepokewa, lakini vilevile zinapatikana ahaadeeth zilizo swaheeh kutoka kwa Ibn 'Umar na Maswahaba yakwamba walifanya hivyo. Amesema al-Haakim: "Sunnah hii imetekelezwa na ahl-il hadeeth. Maalik, Ahmad, Is-haaq na Abu Thaur [wamenukuu matamshi yao kuhusiana na mas'ala hayo]."

Baadhi wamesema yakwamba Takbeeraat huanzia usiku wa kabla ya 'Eid, pindi uonekanapo mwezi, mpaka mtu endapo kwenye Musallaa na atakapowasili Imaam.

Muda wa Takbeeraat katika 'Eid ul-Adh-ha ni kuanzia siku ya Arafah mpaka wakati wa 'Asr katika siku ya kumi na tatu ya Dhul-Hijjah [Angalia Sharh us-Sunnah: vol. 4, Uk. 300-1. Angalia katika Zaad ul-Ma'aad: vol. 1, Uk. 449].

Amesema Imaam al-Bukhaari katika kitabu chake Swaheeh ul-Bukhaari: Vol.2, Uk.45, Mlango 11, "Fadhla za kutenda mambo mema ya masiku ya Tashreeq (11th, 12th, 13th, of Thul-Hijjah). Ibn Abbaas alisoma aya Tukufu, **"... Na kulitaja jina la Allaah katika siku zinazojulikana..."** [yaani; masiku ya mwanzo katika mwezi wa Dhul-Hijjah] na pia masiku ya kuhesabika, yaani; masiku ya Tashreeq. Ibn 'Umar na Abu Hurairah walikuwa wakitoka na kuelekea Sokoni na huku wakisoma Takbeer katika masiku kumi ya mwanzo wa Dhul-Hijjah na watu wakawa wanafuatiliza kusoma Takbeer baada yao. Muhammad bin Ali alikuwa akisoma Takbeer baada ya Nawaafil. Ibn Hajar ameandika katika Fat-hul Baaree: "Hakuna katika hayo kilichothubutu kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Riwaya iliyoswihi kutoka kwa Maswahaba ni ya Ali na Ibn Mas'ud walikuwa wakisoma Takbeeraat kuanzia siku ya Arafah mpaka wakati wa 'Asr ya siku ya mwisho ya Mina [wamepokea Ibn al-Mundhir na wengineo]. Ashaafi'ee, Ahmad, Abu Yusuf na Muhammad wamefuata riwaya hiyo na vilevile ni rai ya 'Umar na Ibn Abbaas."

Hakuna nyakati maalum za kuleta Takbeeraat katika masiku ya Tashreeq (siku tatu baada ya 'Eid ul-Adh-ha). Kwa hakika, inapendekezwa kusoma Takbeeraat katika kila wakati wa masiku hayo.

Imaam al-Bukhaari ameipokea kwenye Swaheeh yake vol. 2, Uk. 46, mlango wa 12. "Wakati wa 'Umar alipokuwa akikaa Mina, alikuwa akisoma Takbeeraat ndani ya hema lake [kwa sauti kubwa] kiasi cha kwamba watu walikuwa wakimsikiya Msikini na wao wakawa ni wenye kumfuatiza. Vilevile watu wa msikitini wakamuigiza mpaka Mina nzima ikawa inanguruma kwa Takbeeraat. Ibn 'Umar alikuwa akisoma Takbeeraat katika masiku hayo ya Mina baada ya swala na alipokuwa kwenye kitanda chake, ndani ya hema lake, alipokuwa amekaa na haliyakuwa anatembea katika masiku hayo yote. Maymunah alikuwa akisoma Takbeeraat katika siku za 'Eid ul-Adh-ha. Wanawake walikuwa wakisoma Takbeeraat nyuma ya Abbaan ibn 'Uthmaan and 'Umar ibn 'Abdulaziz pamoja na wanaume msikitini katika masiku ya Tashreeq."

Al-Haafidh Ibn Hajar amesema: "Riwaya hizi zinaonyesha yakwamba Takbeeraat husomwa katika wakati wote wa masiku haya, baada ya swala na wakati wote.

NJIA TAFAUTI ZA KUSOMA TAKBEERAAT

Takbeeraat hizi zinaweza kusomwa kwa njia nyingi tafauti. Zilizoswihi zaidi ni zile zilizonukuliwa kwa njia iliyo swaheeh na Abdurrazzaaq kutoka kwa Salmaan, aliyesema: "Walikuwa wakisoma Takbeeraat kwa:

'Allaahu akbar, Allaahu akbar, Allaahu akbar kabeera."'

Kutoka kwa Umar na Ibn Mas'ud, yafuatayo yamepokewa: "Allaahu akbar, Allaahu Akbar. Laa ilaaha illa Llaah. Allaahu akbar. Allaahu akbar wa lillahil-hamd." [Angalia katika Sharh us-sunnah: vol. 4, Uk. 301. Angalia Zaadul Ma'aad: vol. 1, Uk. 449.]

2. WANAWAKE NA WATOTO KUTOKA NA KUHUDHURIA SWALA YA 'EID

Shariya inawashurutisha wanawake na watoto watoke na kuhudhuria Swalaatul 'Eidayn. Wanahusika hapo wanawake walio olewa, wasichana ambao hawajaolewa, wanawake mabikra, wazee au wanawake walio kwenye ada zao za mwezi. Umm Atiyyah amepokewa kusema: "Tuliamrishwa kutoka pamoja na wanawake wasichana na walio kwenye ada zao za mwezi kwenda kuhudhuria 'Eid mbili ili nao washuhudie wema na maombi ya Waislamu. Wanawake walio kwenye ada zao za mwezi wanatakiwa kuwa kando na wenzao." [al-Bukhaari vol. 2, Uk. 48, no. 91].

Hadeeth hiyo hapo juu imeweka wazi yakwamba mwanamke aliye kwenye ada yake ya mwezi hawatoswali na watajitenga kando [al-Bukhaari vol. 2, Uk. 52, no. 97]

Ibn Abbaas amepokewa kusema: "Nilitoka pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika siku ya 'Eid ul-Fitr au 'Eid ul-Adh-ha, akaswali na kutoa khutbah, kisha akenda kwa wanawake na akawahutubia, akawakumbusha kuhusu Allaah na akawaamrisha watoe swadaka. [al-Bukhari: vol. 2, Uk. 48, no. 92.]

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

3. KUCHUKUA NJIA TAFAUTI KATIKA KWENDA NA KURUDI KWENYE MUSALLA

Ni rai ya wanavyuoni wengi yakwamba inapendekezwa kwa mtu kwenda kwenye swala kwa njia moja na kisha kurudi nyumbani kwa kutumia njia nyengine, pasi na kujali iwapo atakuwa ni Imaam au asiyekuwa Imaam.

Amepokea Jaabir: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akichukuwa njia tafauti katika masiku ya 'Eid." [Swaheeh al-Bukhari: vol. 2, Uk. 54, no. 102.]

Amesema Abu Hurairah (رضي الله عنه): "Alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akenda kuswali 'Eid, alikuwa akirudi nyumbani kwa kutumia njia tafauti." [Swaheeh Sunan At-Titmthee: vol. 1, Uk. 168, no. 446] .

4. WAKATI WA SWALA ZA 'EID

Wakati wa swala ya 'Eid huanzia tangu jua likichomoza na kupanda juu kiasi cha mita 3 mpaka litakapolingana na kustawi [wakati wa adhuhuri]. Idadi kubwa ya wanavyuoni wamesema yakwamba wakati wa swala ya 'Eid huanzia tangu jua linapochomoza na kuanza kupanda kiasi cha mkuki, kama uonekanavyo kwa macho makavu, na kuendelea hadi jua litakapokurubia kiwango chake cha juu kabisa. Ni bora kuswali swala ya 'Eid kabla ya kuingia mchana katika masaa ya mapema baada ya kuchomoza kwa jua. Sababu ni kwamba watu wapate kwenda kuchinja katika siku ya kuchinja. Kwahiyo, swala katika matukio hayo ('Eid ul-Adh-ha) na iswaliwe mapema kuliko swala katika siku ya 'Eid ul-Fitr.

Amesema Yazeed Ibn Khumayr Rahbee: 'Abdullaah Ibn Busr, Swahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuja pamoja na watu katika siku ya 'Eid ul-Fitr au 'Eid ul-Adh-ha (kwa ajili ya kuswali). Alichukizwa na kuchelewa kwa Imaam, na akasema: Tulikuwa tukimaliza swala yetu ya 'Eid wakati huu, yaani, katika wakati wa kabla ya adhuhuri. [Sunan Abu Dawud: (Eng): vol.1, Uk.293, no. 1131 na ikathibitishwa na Al-Albaanee katika Swaheeh Sunan Aboo Daawood: vol.1, Uk. 210-1, no. 1005. Imaam al-Bukhaari ametaja katika swaheeh yake vol. 2, Uk. 44, mlango 10].

Amesema Ibn Qudaamah: "Ni Sunnah kuiswali swalaat ul-Adh-ha mapema ili kuwaruhusu watu wakati zaidi kutekeleza uchinjaji, na swalaat ul-Fitr na icheleweshwe kidogo kwa ajili ya kuwapa watu nafasi ya kulipa zakaatu ul-Fitr. Mimi sioni ikhtilafu yoyote ya maoni niijuayo kuhusiana na mas'ala haya." [Al-Mughnaee cha Imaam ibn Qudaamah: vol. 2, Uk. 224.]

5. ADHAAN NA IQAAMAH KATIKA SWALA ZA 'EID

Ameandika Imaam Ibn al-Qayyim (رحمه الله): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokwenda katika musalla, alikuwa akiswali pasi na kuadhiniwa wala ku-Qimiwa na wala bila ya "**AS-SWALAATUL JAAMI'AH"**. Sunnah ni kutofanya lolote katika hayo." [Zaadul Ma'aad; vol.1, Uk.442] Ibn Abbaas pamoja na Jaabir (رضي الله عنهم), wote wawili wamesema yakwamba hakuna Adhaan katika siku ya al-Fitr au siku ya al-Adh-ha. [al-Bukhaari; vol.2, Uk.41, No. 78. na Muslim: vol.2, Uk.417, No. 1927].

JINSI YA KUISWALI SWALA YA 'EID.

Inamlazimu kila Muislamu kuswali swala ya 'Eid, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliiswali swala hiyo. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Swalini kama munavyoniona mimi nikiswali." [al-Bukhaari vol.1, Uk.345, No. 604].

1. SUNNAH KABLA AU BAADA YA SWALA YA 'EID

Haikuthubutu kuwepo na swala yoyote ya Sunnah kabla au baada ya swala ya 'Eid. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kuswali swala zozote kama hizo, wala hawakuwahi Maswahaba zake pindi walipowasili kwenye musalla.

Walivyokuwa wakifanya Waislamu katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba hawakuwa wakiswali Sunnah yoyote au swala ya nafl kabla au baada ya swala ya 'Eid.

Amesema Abdullaah Ibn Abbaas: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali swala ya raka'a mbili katika siku ya 'Eid ul-Fitr na wala hakuswali swala yoyote kabla wala baada yake. [Al-Bukhari: vol. 2, Uk. 43, no.81].

2. TAKBEER KATIKA SWALAATUL 'EIDAYN

Swala ya 'Eid ina raka'a mbili na ndani yake ni Sunnah kutamka takbeer mara saba, baada ya takbeer ya ufunguzi na kabla ya usomaji wa Qur'an katika raka'a ya kwanza. Amesema 'Umar (رضي الله عنه): "Swala ya 'Eid ul-Adh-ha ni raka'a mbili kamili, bila ya kufupishwa. Haya ni kulingana na maneno ya Mtume wenu (صلى الله عليه وسلم), na mtu mrongo ameangamia." [al-Irwaa ul-Ghaleel cha Al-Albaanee: vol. 3, Uk.105-6, no. 638]. Katika raka'a ya pili, mtu husoma takbeer mara tano baada ya takbeer ya kawaida kusomwa ya kusimama baada ya sijdah. Tafauti iliyoko baina ya swala ya 'Eid na Ijumaa ni kwamba, katika swala ya 'Eid, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliongeza takbeer mara kumi na mbili, haliyakuwa katika swala ya Ijumaa haifanywi hivyo. Takbeer huregelewa kwa mara saba katika raka'a ya kwanza na mara tano katika raka'a ya pili. Usomaji wa Qur'an huanzishwa baada ya kukamilisha takbeer saba katika raka'a ya kwanza na mara tano katika raka'a ya pili.

TANBEEH: Si katika Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kuinua mikono haliyakuwa unasoma takbeer za nyongeza na hapana chenye kusomwa isipokuwa takbeer. [Tamaamul Minnah; cha Sheikh al-Albaani Uk. 348-9]. Imaam ash-Shawkaani amesema yakwamba rai iliyo na nguvu zaidi ni kwamba iwapo mtu hatosoma takbeeraat kutokana na kusahau, hapasi kufanya sijda ya kusahau. [Naylul Awtwaar; vol.3, Uk.300].

3. USOMAJI WA QUR'AN KATIKA SWALA ZA 'EID

Haikushurutishwa yakwamba ni lazima mtu asome sura ma'lum katika swala ya 'Eid. Imependekezwa (mustahabb) yakwamba katika swala ya 'Eid, Imaam na asome Suratu-Qaaf na Surat ul-Qamar, kama ilivyopokewa yakwamba, 'Umar ibn al-Khattaab alimuuliza Abu Waaqid al-Laythee, "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amezoea kusoma sura gani katika swala ya 'Eid ul-Adh-ha na 'Eid ul-Fitr? Akamjibu: "Alikuwa amezoea kusoma Qaaf Wa'l-Qur'aan al-Majeed [Qaaf 50:1] na Iqtarabat as-Saa'ah wan-shaqq al-Qamar [al-Qamar 54:1]. [Swaheeh Muslim: vol.2, Uk.419, No.1936]. Riwaya nyingi zinaeleza yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisoma Soorat al-A'laa [87] na Soorat al-Ghaashiyah [88] kama alivyokuwa akisoma kwenye swala ya Ijumaa. Amesema an-Nu'maan ibn Basheer: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisoma katika swala za 'Eid mbili na katika swala ya Ijumaa Sabbi Hisma rabbika'l a'laa [al-A'laa 87:1] na Hal ataaka hadeeth ul-Ghaashiyah [al-Ghaashiyah 88:1]." [Swaheeh Muslim: vol. 2, Uk. 414, no.1907]

4. KHUTBAH YA SWALAAT UL-'EID

Khutbah baada ya swalaat ul-'Eid ni Sunnah na pia kuisikiliza. Si lazima kama ilivyo hali ya swala ya Ijumaa. Inaruhusiwa kujirudia nyumbani bila ya kuhudhuria khutbah ya 'Eid. Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni kutoa khutbah baada ya swalaatul 'Eid [Al-Mughnee: vol. 2, Uk. 246]

(Endelea kutoka Uk. 3)

Amesema Abu Sa'eed: "Katika siku ya 'Eid ul-Fitr na 'Eid ul-Adh-ha, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akenda katika musalla na kuanzia na swala na anapomaliza alikuwa akiwaelekea watu, wakiwa watu wamekaa kwenye swafu zao, akiwahutubia, na kuwanasihi na kuwahimiza [kufanya mema]. Na apendapo kutuma jeshi au kuamrisha jambo, alikuwa akifanya hivyo na kisha huondoka."

Abdullaah ibn as-Sa'ib amesema: "Niliswali swala ya 'Eid pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na pindi amalizapo kuswalisha alikuwa akisema: 'Tutatoa khutbah. Yoyote atakaekaa kusikiliza khutbah, na akae. Na yoyote atakae kuondoka na aondoke." [Abu Dawud: (Eng.) vol. 1, Uk. 298, no. 1151, Swaheeh Sunan Abu Daawud: vol.1, Uk.214, no.1024]

Ameandika Ibn al-Qayyim: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akianza khutbah zake zote kwa kumtukuza Allaah na hakuna hadeeth kutoka kwake isemayo yakwamba alikuwa akianza khutba zake za 'Eid kwa takbeer. Ibn Maajah amepokea katika sunan yake kutoka kwa Sa'eed, muadhini wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisoma takbeer katika khutbah zake na hata akizidisha katika khutbah za 'Eid. Juu ya yote hayo, hili halijawa ni dalili yakwamba alianza khutbah (na takbeer)!

Watu wamekhitilafiana kuhusu mwanzo wa 'Eid na khutbah ya Swalaatul Istisqaa' (swala ya mvua). Baadhi yao wanasema yakwamba wanatakiwa waanze kwa takbeer. Baadhi yao wanasema yakwamba khutbah ya swalaatul Istisqaa' huanza kwa kuomba maghfirah haliyakuwa wengine wamesema huanzia na Kumsifu Allaah."

Sheikh ul-Islam Ibn Taymiyyah amesema: "Hilo ni sawa kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Jambo lolote lisiloanza kwa kumsifu Allaah huwa ni pungufu.' Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akitanguliza mazungumzo yake yote kwa kumsifu Allaah. Kuhusu matamshi ya *ma-fuqahaa* wengi, yaani; alikuwa akianza swala ya mvua kwa kuomba Maghfirah kutoka kwa Allaah na khutbah ya 'Eid kwa takbeer, hakuna dalili yake kabisa katika sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa hakika sunnah inakhalifiana na maneno hayo kwani alikuwa akitanguliza mazungumzo yake yote kwa kumsifu Allaah." [Zaadul Ma'aad:vol.1, Uk.447-8]

5. KUPONGEZANA KATIKA MASIKU YA 'EID

Watu wanaweza kubadilishana pongezi na maamkuzi mazuri katika siku za 'Eid, pasi na kujali sampuli ya matamshi yawayo. Kwa mfano wanaweza kuambizana, "Taqabbal Allaahu minnaa wa minkum (Twamuomba Allaah atukubalie [funga zetu na 'Ibada] sisi na nyinyi" au "Eid Mubarak" na maamkuzi mengine yenye kukubalika na yenye kufanana na hayo. [Al-Mughnee: cha ibn Qudaamah: vol. 2, Uk. 259].

Amesema Jubayr ibn Nufayr: "Katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), watu walipokuwa wakikutana katika siku ya 'Eid, walikuwa wakisema, 'Taqabbal Allaahu minnaa wa minka.'" (Ibn Hajar. Isnaad yake ni hasan. Fat-hul Baaree: vol.2, Uk. 446).

Jambo hili la kuamkuana lilikuwa ni maarufu katika zama za Maswahaba na wanavyuoni mfano wa Imaam Ahmad na wengine wameliruhusu. Kuna riwaya zenye kuashiriya yakwamba inaruhusiwa kuwapongeza watu katika matukio maalum. Maswahaba walikuwa wakipongezana pindi kutokeapo jambo zuri, kama vile Allaah anapokubali toba ya mja na kadhaalika. Hapana shaka yakwamba kupongezana kwa njia hii ni mojawapo ya njia za heshima kubwa za adabu na mojawapo ya tabia nzuri za kijamii miongoni mwa Waislamu.

Kwa uchache kabisa, unaweza kurudisha maamkuzi ya 'Eid pindi utakapoamkuliwa, na ubakie kimya iwapo hakutosemwa kitu, kama alivyosema Imaam Ahmad (رحمه الله): "Mtu anaponiamkuwa, mimi humrudishia maamkuzi, lakini sianzi maamkuzi yenyewe."

6. MWENYE KUKOSA SWALA YA JAMAA YA 'EID ANAWEZA KUSWALI RAKAA' MBILI

Katika swaheeh al-Bukhaari, tunaona kwenye mlango uitwao: "Yoyote mwenye kukosa swala ya 'Eid na aswali raka'a mbili, na vilevile wanawake na wale wenye kubakia majumbani na vijijini na wafanye hivyo, kwani imethubutu kwa matamshi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Enyi Waislamu, hii ni 'Eid yetu." Anas ibn Maalik alipokuwa az-Zaawiyah alimuamrisha mtumwa wake ibn Abee Ghaniyyah awakusanye jamii yake (Anas) na kizazi chake. Anas akaongoza swala inayofanana na ile inayoswaliwa na watu wa Mjini na akasoma takbeer zenye kufanana na takbeer zao. Ikrimah akasema: "Watu wa vijijini na wakusanyike pamoja katika siku ya 'Eid na waswali raka'a mbili kama afanyavyo Imaam."

Amesema 'Ataa', "Yoyote atakaekosa swala ya 'Eid na aswali raka'a mbili." [Swaheeh al-Buukhari: vol. 2, Uk. 55, mlango. 25]

7. KUILIPA SWALA YA 'EID KATIKA SIKU IFUATAYO

Amepokea Abu 'Umair ibn Anas: "Wajomba zangu ma-Answaari katika Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) waliniambia, 'Mwezi wa Shawwal ulifichikana kwetu sisi, na kwahivyo, wenzetu wakafunga. Kisha mwishoni mwa siku, wenye vipando wakaja na wakashuhudia mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba wameuona mwezi katika usiku uliotangulia. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaamrisha watu wafungue saumu zao na watoke na kuelekea kwenye musalla siku ifuatayo." Katika hadeeth hii, kuna ushahidi kwa wale wenye kusema yakwamba iwapo watu watakosa swalaatul 'Eid kutokana na baadhi ya udhuru, basi wanaweza kwenda na kuswali katika siku ifuatayo.

8. KUCHEZA, KUJISTAREHESHA, KUIMBA NA KULA KATIKA SIKU YA 'EID

Mambo haya, iwapo yatahifadhiwa ndani ya mipaka ya kisheriya, yanaruhusiwa katika siku ya 'Eid. Imepokewa kutoka kwa Anas: "Pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuja Mjini Madinah, walikuwa na siku mbili za michezo na kujistarehesha. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: 'Allaah (سبحانه وتعالى) amewabadilishia siku hizo kwa siku mbili zilizo bora kuliko hizo: siku ya al-Fitr na siku ya al-Adh-ha." An-Nasaaee: (Eng.): vol.2, Uk. 333, no. 1559 Swaheeh Sunan An-Nasaaee: vol. 1, Uk. 341, no. 1465].

Amesema 'Aishah: "Mahabashi walikuwa wakionyesha uhodari wao msikitini katika siku ya 'Eid. Nikawaangalia kupitia kwenye mabega ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akayashusha chini kidogo ili nipate kuwaona kwa vizuri zaidi mpaka nikatosheka." [Swaheeh al-Bukhari: vol.1, Uk. 265, no. 445. Swaheeh Muslim: vol. 2, Uk. 421, no.1943]

Swaheeh al-Bukhari, na Swaheeh Muslim vilevile amepokea kuwa alisema: "Aboo Bakr alituingilia katika siku ya 'Eid na palikuwa na vijakazi waliokuwa wakiimba vita vya kivita Bu'ath ambapo wengi wa ma-Aus na ma-Khazraj waliuwawa. Abu Bakr akasema: 'Enyi waja wa Allaah, nyinyi munachezea zumari za Mashetwani!' Akasema mara tatu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: " 'Ewe Abu Bakr, kila watu huwa na sherehe na hizi ni sherehe zetu."

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]